Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam

JARIDA LA UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU YA TAMISEMI

# MIUNDOMBINU NA MAENDELEO

Toleo la 1

Mei, 2018




## Uzinduzi wa Jengo la Mradi wa DMDP, Manispaa ya Temeke



***Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe.Selemani S.Jafo(katikati) akikata utepe kuzindua Jengo la Utawala na Maabara za Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es salaam katika Manispaa ya Temeke. Kutoka kulia ni mratibu wa miradi inayofadhiliwa na Benki ya Dunia Eng.Davis Shemangale, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam Theresia Mbando na Mkuu wa Wilaya ya Temeke Mhe. Felix Lyaniva,kutoka kushoto ni Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke Nassib Mmbaga na Mbunge wa Temeke Mhe. Issa Mangungu***




***Jarida hili limeandaliwa kwa ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP).***

.

*Jarida hili ni maoni ya mtayarishaji,.*

DMDP
Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam

# BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
***Eng. Mussa Iyombe***
***Katibu Mkuu – Ofisi ya Rais, TAMISEMI***

**Wajumbe**
***Eng. Davis Shemangale***
***Eng. Emmanuel Ndyamukama***
***Eng. Hezron Kilamhama***
***Eng. Gilbert Mfinanga***


**Waandishi**
***Rafael Kilapilo***
***Nteghenjwa Hosseah***
***Angela Msimbira***


**Mhariri Mkuu**
***Rafael Kilapilo***

**Wahariri Wasaidizi**
***Nteghenjwa Hosseah***
***Angela Msimbira***

**Msanifu Jarida**
***Nteghenjwa Hosseah***

**Jarida hili hutolewa na:**
***Ofisi ya Rais,***
***Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa -TAMISEMI kwa kushirikiana na DMDP***
***S.L.P 1923***
***Dodoma-Tanzania***
***Simu: (+255) 26 -2321234***
***Barua pepe: ps@tamisemi.go.tz***
***Tovuti: www.tamisemi.go.tz***





# YALIYOMO


- Tahariri
- Uboreshaji wa Jiji la Dar es Salaam ni wa Lazima
- Waziri Jafo aipongeza Manispaa ya Temeke
- Serikali Kufanya Uwekezaji Mkubwa Korido ya Mabasi Yaendeyo Haraka
- Jafo - Zingatieni Ubora Kuepuka Wakandarasi Wababaishaji
- Changamoto ya Miundombinu Kinondoni yapata Mwarubaini
- Umakini Wahimizwa Tathmini ya Mradi wa DMDP
- Dondoo Muhimu za Mradi
- DMDP Kuwaondolea Kero ya Maeneo Wamachinga
- Dondoo Muhimu za Mradi
- Matukio katika Picha






*TAHARIRI:*

# Jiji la Dar es salaam kuendelezwa Kimkakati



Eng. Mussa Iyombe
Katibu Mkuu, OR—TAMISEMI

**KWA MARA YA KWANZA niwakaribishe wasomaji wetu katika toleo la kwanza la Jarida la Miundombinu na Maendeleo ambalo linaelezea kwa undani kazi zinazofanyika kupitia mradi wa uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP).**

**Mradi huu unatekelezwa na Serikali ya Tanzania kupitia fedha za Mkopo kutoka Benki ya Dunia na wadau wa maendeleo,. Mradi umejikita katika kutatua changamoto ambazo kwa namna moja ama nyingine kwa kipindi kirefu zimekuwa zikikwamisha shughuli za maendeleo katika Jiji la Dar es salaam. Serikali kwa kutambua hilo imechukua jitihada za makusudi kuleta mradi huu utakaopunguza changamoto zinazomkwaza mwananchi wa Jiji hili.**

**Mradi wa *DMDP* utaendeleza Jiji kimkakati na utagusa maeneo muhimu ambayo yataleta mabadiliko ya haraka.**

**Utekelezaji wa mradi huu utajikita zaidi kwenye miundombinu kuanzia ujenzi barabara, madaraja na makalavati, mifereji ya kusafirishia maji ya mvua, uwekaji wa taa za barabarani, uboreshaji wa kingo za mito, maeneo ya kupumzikia, masoko, uboreshaji wa bonde la mto msimbazi, uendelezaji wa ukanda wa mabasi haraka, stendi za daladala, uboreshaji wa makazi yasiyopangwa, ujenzi wa mji wa kisasa, viwanja vya michezo na kuzijengea uwezo Halmashauri wa ukusanyaji wa mapato ya ndani .**

**Kazi zote hizi zinamgusa mwananchi kuanzia wa chini kabisa, kati hadi mweye uwezo wa juu. Mradi huu utafungua fursa za kibiashara na kiuchumi hatimaye kuleta maendeleo kwa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.**

***Karibu sana usome Jarida hili.***

# Dar Mpya Yatengenezwa

*Na Mwandishi wetu*

**JIJI** la Dar es Salaam, limekuwa likichangia kwa asilimia kubwa katika ukuaji wa pato la Taifa na kuwa lango la biashara kwa mataifa ya jirani lakini bado linakabiliwa na changamoto ya miundombinu.

Inakadiriwa kuwa, asilimia 70 ya makazi ya jiji la Dar es Salaam hayajapangwa na msongamano wa magari na athari za mafuriko wakati wa mvua katika baadhi ya maeneo imekuwa ni changamoto zinazowakabili wakazi wake kwa kipindi kirefu.

Serikali kwa kuliona hilo, imebuni mradi ujulikanao kama Uendelezaji wa Jiji la Dar es salaam "***Dar es Salaam Metropolitan Development Project***" (DMDP) ambao ni miongoni mwa miradi mingine mingi ya uboreshaji wa miundombinu na huduma za kijamii yenye lengo la kuboresha maisha ya watanzania.

Mradi wa DMDP, unatekelezwa na Serikali katika Halmashauri tatu za Ilala, Temeke na Kinondoni ili kukabiliana na changamoto ya ubovu wa miundombinu.

Benki ya Dunia imetoa mkopo nafuu kwa Serikali wa USD 300 milioni ambazo ni takribani Tsh . Bil 660 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na Shirika la Maendeleo la Nchi za Nodric limetoa USD Mil. Tano (5) ambazo ni ruzuku kwa Serikali kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabia ya Nchi.



***Ujenzi Unaendelea: Daraja la Toangoma ni kiunganishi muhimu kwa wakazi wa Kijichi,Temeke na Kigamboni lakini kwa muda mrefu wananchi hao hawakua na Daraja la Uhakika kupitia DMDP changamoto hiyo imetatuliwa.***

Aidha Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la Maendeleo la "DFID" limechangia ruzuku ya USD Mil. 20 katika kuboresha Bonde la Mto Msimbazi chini ya Mpango wa '*Tanzania Urban Resilience Programme*'.

Serikali inachangia Dola milioni 25.20 kwa ajili ya kulipa fidia kwa wakazi watakaoathirika na mradi huo.

Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI, Mhe. Selemani Jafo, anasema mradi huu pamoja na mambo mengine umelenga kuiwezesha Serikali kutoa huduma yake kwa jamii kwa kuboresha miundombinu msingi na kujenga uwezo wa Manispaa za Jiji la Dar es Salaam.

**Inaendelea Uk………..10**

# Waziri Jafo aipongeza Manispaa ya Temeke

*Nteghenjwa Hosseah, OR TAMISEMI*

**WAZIRI** wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Selemani Jafo amepongeza uongozi wa Manispaa ya Temeke kwa usimamizi mzuri wa miradi ya maendeleo na maagizo mbalimbali ya Serikali.

Waziri Jafo aliyasema hayo wakati wa ufunguzi wa Jengo la Utawala na Maabara itakalotumiwa na wataalam wa mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam(DMDP) kutekeleza shughuli mbalimbali za mradi mpaka hapo utakapokamilika.

Alisema kuwa Mradi huo unatekelezwa katika Manispaa zote za Jiji la Dar es salaam lakini Manispaa ya Temeke imekuwa ya kwanza kukamilisha jengo hili ambalo analifungua rasmi ili lianze kutumika kwa kazi mbalimbali za mradi.

“Temeke sio tu mmetekeleza kwa ufanisi mradi huu lakini hata maagizo mbalimbali yanayotolewa na viongozi wa Serikali , mimi mwenyewe ni shahidi kwa sababu nilishapita zaidi ya mara tatu na kuagiza kazi mbalimbali ninaporudi baada ya siku kadhaa nakuta mmetekeleza kwa kiwango kinachostahili” alisema Jaffo.

Waziri Jafo aliwataka viongozi wa Manispaa zingine kuja kujifunza kutoka Manispaa ya Temeke namna ambavyo wamekuwa makini kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mradiwa Uendeezaji wa Jiji la Dar es Salaam unatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano na utahusisha ujenzi wa barabara kilometa 210 kwa kiwango cha lami kwenye maeneo mbalimbali yanayounganishwa na ukanda wa mabasi yaendayo haraka, maeneo yanayounganisha Wilaya na mkoa kwa ujumla pamoja na maeneo yaliyojengwa kiholela kwenye kata 14 zilizoainishwa.



**Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe.Selemani Jafo akizungumza na hadhara(haipo pichani) wakati wa ufunguzi wa Jengo la Utawala la mradi wa “*DMDP*” Manispaa ya Temeke.**

Mradi huu pia utajenga Km 40 za mifereji mikubwa ya kutiririsha maji ya mvua ili kudhibiti changamoto za mafuriko ujenzi wa ofisi tatu za kudumu zenye gorofa moja katika Manispaa za Ilala, Temeke na Kinondoni pamoja na maabara za kisasa za kupima viwango vya ujenzi pamoja na ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kutunza mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato na mifumo ya upimaji na utunzaji wa taarifa za kijiografia (GIS).

Zaidi ya hapo DMDP itapandisha hadhi maeneo yaliyojengwa kiholela katika kata 14 za Tandale, Mburahati, Mwananyamala, Gongo la Mboto, Kiwalani, Ukonga, Keko, Kilakala, Mbagala kuu, Mbagala, Mtoni, Yombo vituka, Kijichi na Makangarawe.

Huduma zitakazopelekwa katika kata hizo ni uwekaji wa taa za barabarani, ujenzi wa mifereji ya kutitirisha maji, njia za watembea kwa miguu, kuweka nyenzo za ukusanyaji taka ngumu kwa kununua magari ya kuzoa taka na ununuzi wa vizimba vya taka, ujenzi wa masoko, vituo vya mabasi, maeneo ya kupumzikia, huduma za vyoo vya umma na huduma za maji safi pamoja na upimaji wa viwanja zaidi 800 vyenye miundombinu ya kijamii katika eneo la Vikunai kata ya Twangoma Manispaa ya Temeke.

Halkadhalika Mradi utasaidia kuimarisha uwezo wa kitaasisi wa Manispaa za jiji la Dar es salaam kwa kuboresha Mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani, kuainisha na kuibua miradi jumuishi ya njia za usafirishaji jijini na matumizi bora ya ardhi kwa kuibua aina mbalimbali za vivutio vya uwekezaji katika ukanda wa mabasi yaendayo haraka, kuimarisha mifumo ya ujenzi na matengenezo pamoja na kuimarisha mifumo ya mipango miji katika ngazi zote kwenye Manispaa za jiji; Kuandaa na kutekeleza Mpango Kabambe wa Mfumo wa Maji Taka na Maji ya Mvua katika mkoa wa Dar es salaam *(Dar es Salaam Drainage and Sewerage Master Plan 2016 -2036).*

Aidha, mradi utasaidia kujenga uwezo kwa manispaa katika usimamizi wa miradi mikubwa hasa kwenye nyanja za manunuzi, usimamizi wa fedha, masuala ya mazingira, ukaguzi, ufuatiliaji na tathmini.

# Serikali Kufanya Uwekezaji Mkubwa Korido ya Mabasi Yaendeyo Haraka

*Angela Msimbira, OR-TAMISEMI*

**MKURUGENZI** wa Idara ya Uendelezaji Miji, OR-TAMISEMI Dkt. Mkuki Hante amesema Serikali inampango wa kufanya uwekezaji mkubwa katika Ukanda wa mabasi yandayo haraka ambao utaimarisha uchumi kuanzia kwa wananchi wa chini mpaka wale wa hali nya juu.

Akitoa salaam kwa niaba ya Katibu Mkuu OR-TAMISEMI wakati wa kupokea taarifa toka kwa wataalam washauri wa kampuni ya "Broadway Malyan" waliopewa kazi ya tengeneza mpango wa matumizi bora ya ardhi katika Ukanda wa mabasi yaendayo haraka ikiwa ni sehemu ya mradi wa uendelezaji Jiji wa Dar-es-salaam (DMDP) unaosimamiwa na OR-TAMISEMI Dkt. Hante amesema Serikali imeweka mikakati ya kufanya mji wa Dar-es-salaam kuwa kitovu cha uchumi wa nchi kwa kuwekeza katika ujenzi miundombinu itakayowavutia wawekezaji wa Ndani na Nje.

Amesema kuwa uwekezaji unaofanywa na Serikali kwa Fedha za Mkopo toka Benki ya Dunia una lengo la kuleta mabadiliko katika Ukanda wa mabasi hayo ambao utarahisha shughuli za kila siku za mwananchi wa kawaida na wakati huo huo kuwaongezea kipato.

Akizungumzia mpango uliowasilishwa katika kikao hicho Dkt. Hante anafafanua kuwa lengo la kuonyesha namna ambayo Ukandawa mabasi yaendayo haraka utakavyokuwa baada ya uwekezaji huku ukizingatia Sheria za Mipango Miji zilizopo na matumizi bora ya Ardhi.

"Eneo kubwa la Jiji la Dar-es-Salaam halijapangwa lakini maeneo yote yatakayopitiwa na mradi umbali wa mita 500 kutoka barabara Utapangwa kwa Unadhifu ambapo itasaidia kubadilisha Sura ya Mji na kulifanya kuwa Jiji la Kisasa ambalo litaweza kushindana na Majiji mengine duniani alisema Dkt.Hante.

Aliongeza kuwa mpango utakaotengenezwa na wataalam washauri itasaidia kuibua vipaumbele vya uwekezaji katika jiji la Da-es-salaam hasa katika korido za mabasi yaendayo haraka na kuona jinsi uendelezaji wa miundombinu hasa katika awamu ya kwanza ambao utasaidia kuleta mabadiliko ya kiuchumi, kijamii na kimazingira.

Uwekezaji huu katika ukanda wa mabasi yaendayo haraka utapita katika Manispaa Nne, Kata 31, Mitaa 101 na utakua na Vituo 32 pia utahusisha makazi yenye watu zaidi ya milioni moja na kutoa ajira kwa wananchi zaidi ya 485.

Aidha mpango huu pia utazingatia ukuaji wa kisasa unaotazamiwa katika Sekta ya Afya, Elimu na miundombinu ambayo haikuwepo hapo awali.

Baada ya kumaliza awamu ya kwanza ya mradi wa Mabasi yaendayo haraka kumeanza kuwa na mvuto wa uwekezaji pembezoni mwa barabara hivyo Serikali imeona ni vyema kuwekeza ili kuongeza fursa kwa wananchi wake na kuleta maendeleo ya haraka.



**Picha 1& 2: Baadhi ya wataalamu na wadau wa Jiji la Dar-es-salaam wakifuatilia mawasilisho ya wataalamu washauri toka kampuni ya Broadway Malyan kuhusu mpango matumizi bora ya ardhi katika ukanda wa Mabasi yaendayo haraka**

Kutoka Uk…….7

**ANASEMA** pia una lenga kuchangia katika kukabili matukio makubwa ya dharula kama majanga ambayo yanaweza kulikabili jiji la Dar es Salaam.

Jafo anasema pia ni kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia ya nchi na kuepuka madhara yanayoweza kuwapata watu.

**MALENGO YA SERIKALI**

Jafo anasema, mpango wa Serikali ifikapo mwaka 2020 watu wanaingia jijini Dar es Salaam wapoteee.

"Natamani ikifika 2020 wageni wanaingia Dar es Salaam, wapotee kwa sababu mazingira ya jiji hili yatakuwa yamebadilika," anasema Jafo.

Anasema kuwapoteza watu wageni wanaoingia katika jiji hilo ni kwa kupitia mradi huo watabadili mazingira na muonekano wa zamani na kuwa na muonekano mpya.

**MRADI WENYEWE**

Utekelezaji wa mradi huo, umepangwa kufanyika na unaendelea kufanyika katika awamu mbili ikiwamo ya kipindi cha kwanza cha miaka mitano kuanzia mwaka 2016 hadi mwaka 2020.

Jafo anasema awamu ya pili ya mradi ni kuanzia mwaka 2020 hadi mwaka 2025 ambayo ni makubaliano kati ya serikali na Benki ya Dunia.

Jafo anasema utekelezaji wa mradi huo awamu ya kwanza ni ujenzi wa barabara kilometa 210 kwa kiwango cha lami kwenye maeneo mbalimbali yanayounganishwa na ukanda wa mabasi yaendayo haraka.

Pia katika maeneo yanayounganisha wilaya na mkoa kwa ujumla pamoja na maeneo yaliyo-



*Uboreshaji wa Miundombinu ya Barabara ukiendelea katika Manispaa ya Temeke kupitia Mradi wa DMDP*

Jafo anasema pia ujenzi wa ofisi tatu zenye maabara za kudumu katika Manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke ambayo imeshakamilika na kukabidhiwa kwa uongozi.

"Ofisi hizi pia zitakuwa na vifaa vya kisasa vya kutunza mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato na mifumo ya upimaji na utunzaji wa taarifa za kijiografia," anasema Jafo.

Anaeleza zaidi kuwa, ujenzi wa kilometa takribani 45 za mifereji mikubwa ya kutiririsha maji ya mvua ili kudhibiti changamoto za mafuriko ni moja ya utekelezaji wa mradi huo.

Pia anasema watapandisha hadhi maeneo yaliyojengwa kiholela katika kata 14 ambazo ni Tandale, Mburahati, Mwananyamala, Gongo la boto, Kiwalani, Ukonga, Keko, Kilakala, Mbagala KUu, Mbagala, Mtoni, Yobo vituka, Kijichi na Makangarawe.

Anasema huduma zitakazotolewa katika kata hizo ni kuweka taa za barabarani, ujenzi wa mifereji ya kutiririshia maji, ujenzi wa njia za watembea kwa miguu na kuweka nyenzo za ukusanyaji taka ngumu.

Jafo anasema pia watanunua magari ya kusomba taka ngumu na ununuzi wa vizimba vya taka, ujenzi wa masoko na ujenzi wa vituo vya mabasi.

Anasema mradi huo, utawezesha kujenga maeneo ya mapumziko, huduma za vyoo vya umma na huduma za maji safi.

Anasema huduma zitakazotolewa katika kata hizo ni kuweka taa za barabarani, ujenzi wa mifereji ya kutiririshia maji, ujenzi wa njia za watembea kwa miguu na kuweka nyenzo za ukusanyaji taka ngumu.

**Inaendelea uk ……..13**

# Jafo - Zingatieni Ubora Kuepuka Wakandarasi

## Rafael Kilapilo, OR-TAMISEMI

**WAZIRI** wa Nchi , OR-TAMISEMI, Mhe. Selemani Jafo amewataka wahandisi na watendaji wa Manispaa za Kinondoni, Ilala na Temeke ambazo zinatekeleza Mradi wa Uendelezji Jiji la Dar es Salaam (DMDP), kuzingatia ubora wa hali ya juu katika ujenzi wa miundombinu na kuepuka kujihusisha na wakandarasi wababaishaji.

Waziri Jafo aliyasema hayo wakati alipofanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya DMDP katika Manispaa ya Kinondoni mapema mwezi Januari, 2018 na kuwataka wasimamizi hao kutokuwa na mjadala au maafikioano kwenye suala zima la ubora wa barabara.

Akizungumza mara baada ya kukagua Jengo la ofisi za mradi pamoja na barabara za Makumbusho - Sokoni, Nzasa na Viwandani, Jafo alisema kuwa barabara za DMDP zinazojengwa ni tofauti sana na barabara zilizokuwa zikijengwa awali, zinajengwa kwa ubora wa hali ya juu na zinagharimu fedha nyingi, hivyo hatarajii kuona baada ya muda zinaanza kuharibika.

"Barabara hizi pamoja na miundombinu mingine katika mradi huu kwa Manispaa za Dar es Salaa kwa ujumla wake zinagharimu kiasi cha fedha takribani Bil. 660. Hizi ni fedha nyingi, sitarajii kuona baada ya mwaka mmoja au miwili tunaaza kuziba viraka. Niwatake wahandisi wetu mnaosimamia barabara hizi kuhakikisha zinakuwa na ubora wa hali ya juu,. Fanya mfanyavyo, sihitaji majadiliano kwenye swala la ubora,".

Aidha Mhe. Jafo aliwataka uongozi wa Halmashauri hizo kuwaondoa haraka wakandarasi ambao wataonekana kukwamisha utekelezaji au kuharibu kazi.

" Sitaki utani kwenye ubora na mkibaini mkandarasi anataka kukwamisha kazi hizi kwa njia moja au nyingine aondolewe mapema sana kabla ya kuharibu kazi" alisema.

Alieleza kuwa nia ya Serikali ni kubadilisha Jiji la Dar es Salaam na kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili wananchi wa jiji hilo kwa muda mrefu.

Waziri Jafo alisema kuwa ataona aibu endapo barabara za jiji la Dar es Salaam zitakosa ubora kama ule ulipo katika barabara za miji ya Tanga, Arusha, Mtwara Mikindani, Kigoma Ujiji, Mbeya, Mwanza na Dodoma ambazo pia zimejengwa kupitia Mradi wa Uendelezaji Miji Kimkakati (TSCP), unaosimamiwa na OR-TAMISEMI.

Aidha, Jafo alimuagiza Mratibu wa Mradi huo katika Manispaa ya Kinondoni, kukamilisha ujenzi wa jengo la ofisi lenye maabara ya kisasa mapema iwezekanavyo ili alizindue kabla ya Februari 19 mwaka huu.

Pia aliagiza kukamilika kwa ujenzi wa barabara ya Makumbusho-Sokoni ili nayo iwekewe jiwe la msingi wakati wa uzinduzi wa jengo la Manispaa kuashiria kuanza rasmi kwa utekelezaji wa Mradi wa DMDP unaotarajiwa kumalizika mwaka 2030.



*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe.Selemani Jafo(mbele) akikagua barabara za Manispaa ya Kinondoni zinazojengwa kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es salaam*



*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe.Selemani Jafo(aliyeinama) akikagua ujenzi wa miundombinu katika barabara ya Makumbusho inayojengwa kupitia mradi wa DMDP*



*Waziri wa Nchi OR-TAMISEMI Mhe.Selemani Jafo (kulia)akitoa maelekezo kwa wataalam wa Manispaa ya Kinondoni baada ya ukaguzi wa miundombinu inayojengwa kupitia*

# Changamoto ya Miundombinu Kinondoni yapata Mwarubaini

***CHANGAMOTO*** ya mafuriko na ubovu wa miundombinu katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni zimeanza kutafutiwa ufumbuzi, kufuatia utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa jiji la Dar es Salaam (DMDP).

Mradi huo ulioanza kutekelezwa nchini mwaka 2015, unaotekelezwa katika Manispaa tatu za jiji hili, kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia na fedha za ndani.

Wananchi wa Manispaa ya Kinondoni ambao nao ni wanufaika wa mradi huu, wanaeleza namna ambavyo Serikali imewasaidia kuondokana na changamoto za miundombinu zilizokuwa zikiwakabili.

Julias Tarimo ni dereva wa daladala zinatoka Makumbusho kuelekea Bunju, anasema kujengwa kwa barabara za kuingia katika stendi hiyo kumepunguza kero kubwa iliyokuwa ikiwakabili.

"Tunaishukuru Serikali kwa kejenga barabara za kuingia katika stendi hii ya daladala ambazo zilikuwa zikisababisha kupata hasara ya kutengeneza magari kila wiki," anasema Tarimo.

Anaeleza kuwa, wakati wa mvua mashimo yalikuwa yakiongezeka na kusababisha maji kutuama na magari kukwama.

Tarimo anasema kujengwa kwa barabara hizo kutasaidia kuokoa muda wa kuingia na kutoka katika stendi hiyo lakini pia usalama wa vyombo vyao vya usafiri.

Naye Jamila Okamu mfanyabishara wa duka la nguo pembezoni mwa barabara hiyo ya kuingia kituo cha Makumbusho, anasema kujengwa kwa barabara hiyo kutawarahisishia kupata huduma muhimu.

Anasema awali walikuwa wakipata shida ya vumbi na kutokana na ubovu wa barabara, wateja wenye magari walishindwa kusimama kununua bidha kwenye maduka yao.

"Tunaishukuru Serikali kwa kutuletea huduma hii muhimu ambayo tulikuwa tukiilalamikia mara kwa mara. Tunaomba kabla ya kumaliza waweke matuta ili kuepusha ajali zitokanazo na mwendo kasi," anasema.

John Julias ni mfanyabishara katika maeneo ya Makumbusho anasema, wanaishukuru Serikali kwa kusikia kilio chao cha siku nyingi.

"Sawa Serikali imetusaidia kujibu maombi yetu lakini bado tunachangamoto ya kupanda kwa gharama za fremu za maduka lakini haya ndio maendeleo yenyewe," anasema.

Innocent Vicent ni kinyozi katika eneo la Mkambusho, anasema kabla ya kujengwa kwa barabara hiyo, magari yaliyokuwa wakipita hadi kwenye vibaraza vya ofisi zao.

"Barabara ilikuwa mbovu hivyo watu walikuwa wakipanda kwenye vibaraza vya maduka yetu na kusababisha usumbufu mkubwa kwetu sisi," anasema.

Kadhalika anasema pia maji yalikuwa yakituama kwenye barabara wakati wa mvua na kusababisha mazingira kuwa machafu.

Inaendelea Uk 16……………………..



***Ujenzi unaendelea wa Soko la Kisasa katika Kata ya Kijichi ambalo litattatua changamoto ya uhaba wa maeneo ya kufanyia biashara kwa wafanyabiashara ndogondogo.***

Kutoka Uk.10



# Kazi inaendele; Ujenzi wa Barabara za Manispaa ya Ilala

**JAFO** anasema pia watanunua magari ya kusomba taka ngumu na ununuzi wa vizimba vya taka, ujenzi wa masoko na ujenzi wa vituo vya mabasi.

Anasema mradi huo, utawezesha kujenga maeneo ya mapumziko, huduma za vyoo vya umma na huduma za maji safi.

Anasema huduma zitakazotolewa katika kata hizo ni kuweka taa za barabarani, ujenzi wa mifereji ya kutiririshia maji, ujenzi wa njia za watembea kwa miguu na kuweka nyenzo za ukusanyaji taka ngumu.

Pia amesema wataimarisha mifumo ya ujenzi wa matengenezo pamoja na kuimarisha mifumo ya mipango miji katika ngazi zote kwenye manispaa za jiji.

Anasema wataandaa na kutengeneza mpango kabambe wa mfumo wa maji taka na maji ya mvua katika mkoa wa Dar es Salaam.

Jafo amesisitiza kupitia mradi huo utasaidia kujenga uwezo wa manispaa katika usimamizi wa miradi mikubwa hasa kwenye Nyanja za manunuzi, usimamizi wa fedha, masuala ya mazingira na ukaguzi , ufuatiliaji na tathimini.

**Namna unavyotekelezwa**

Anasema mradi huo umeanza kwa kuainisha maeneo yasiyohitaji fidia na Manispaa kuingia mikataba na wakandarasi mbalimbali katika maeneo hayo.

Anasema katika maeneo yenye kuhitaji fidia, Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na manispaa za Jiji hilo, inafanya uhakiki wa majendwali ya fidia,

Anasema taratibu za kuwalipa watu fidia zinafanyika na baadhi ya watu katika maeneo ambako mradi umetekelezwa wameshalipwa.

# Umakini Wahimizwa Tathmini ya Mradi wa *DMDP*

**Nteghenjwa Hosseah,**

**OR-TAMISEMI**

**KATIBU** Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhandisi Mussa Iyombe amewataka washiriki wa kikao cha Tathmini ya Utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam "DMDP" kuwa makini katika kuchambua taarifa mbalimbali za mradi zitakazowasilishwa katika kikao hicho.

Akisoma hotuba kwa niaba ya Katibu Mkuu katika kikao hicho Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam Bi. Theresia Mbando amesema kuwa tathmini hii inayofanyika kwa sasa itasaidia kutambua kwa upana wake huku ikilenga vipengelea vyote vine ambavyo vimelengwa kutekelezwa katika mradi huu.

"Mradi huu Mkubwa wenye lengo la kuboresha Jiji la Dar es salaam ili lizidi kuwa bora katika Sekta ya miundombinu, usafiri mjini, usalama, makazi bora sambamba na kujenga uwezo wa Kitaasisi.

Mradi huu pia utaweka mifumo stahiki na ya kutosha kutunza kumbukumbu na takwimu itakayosaidia katika ukusanyaji wa mapato ndio ambao tunajadili hapa leo kuangalia namna wataalamu wetu walivyusimamia na nini kimefanyika kwa kiasi gani na kwa kiwango gani" alisema Bi. Mbando.

Aidha Bi. Mbando aliongeza kuwa anategemea mawazo na hoja za msingi kutoka kwa wadau walioshiriki katika mkutano huo kwa ajili ya kujenga na kuboresha mipango iliyopo ya utekelezaji wa mradi huo.

Katika Kikao hicho mwakilishi wa Benki ya Dunia ambaye pia ndiye Msimamizi Kiongozi wa Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam kutoka Benki ya Dunia Ndg. Erick Dickson alisema kuwa Serikali ya Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia wameleta Mradi utakaobadilisha muonekano wa Jiji la Dar es Salaam.



*Katika Picha ya pamoja ni Katibu Tawala Mkoa wa Dar es salaam Theresia Mbando (katikati) Msimamizi Kiongozi wa DMDP toka Benki ya Dunia Erick Dickson (Pili kushoto), Mkurugenzi wa Idaya ya Uendelezaji Miji OR-TAMISEMI, Mkuki Hante (Kwanza kushoto), Mratibu wa miradi inayotekelezwa na Benki ya Dunia chini ya OR-TAMISEMI Davis Shemangali*

Aliongeza kuwa tunatakiwa kuangalia kwa makini namna ambavyo mradi huu unavyotekelezwa katika kipindi hiki cha Nusu Mwaka; Yale yaliyopangwa yametekelezwa, malengo ya mradi yamefikiwa,wananchi wamenufaikaje kupitia mradi huuna je hakuna athari zozote za kimazingira zilizotokea bila kusahau ushiriki wa wananchi upo kwa kiasi gani.

Katika awamu ya kwanza ya mradi huu ambayo inatekelezwa kwa kipindi cha 2016 - 2020 Mradi utagharimu jumla ya Dola za Kimarekani Milioni 300 ambazo ni Fedha za mradi ambazo ni Fedha za Mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Aidha Shirika la Maendeleo la Nchi za Nordic limetoa ruzuku dola Mil.5 kwa ajili ya kukabiliana na changamoto za Mabadiliko ya Tabia ya Nchi

Wakati huo huo Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la Maendeleo la DFID linachangia ruzuku ya USD Mil. Tano (5) kwa ajili ya kuboresha Bonde la Mto Msimbazi na Serikali ya Tanzania inachangia dola za kimarekani milioni 25 kwa ajili ya ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaoathirika na mradi.

Kikao hicho cha siku tatu kilihusisha wataalamu kutoka Ofisi ya Rais Tamisemi, Wasimamizi wa mradi kutoka Benki ya Dunia, Wataalam kutoka Halmashauri zote za Mkoa wa Dar es salaam pamoja na washauri wa mradi kutoka kampuni mbalimbali zinazofanya kazi za mradi huu.

# DONDOO MUHIMU ZA MRADI

## MANISPAA YA TEMEKE

**I. Ujenzi wa Ofisi ya mradi pamoja na Maabara**

**II. Ujenzi wa barabara 92 kwa kiwango cha lami ya zege (Km 102) katika kata 14**

**III. Ujenzi wa mifereji 20 ya kusafirishia maji ya mvua (Km 100)**

**IV. Uwekaji wa Taa za barabarani kwenye maeneo 14 ya makutano ya barabara yaliyoko kwenye Kata 10**

**V. Ujenzi wa Masoko**

- **Ujenzi wa Soko la Kijichi**
- **Ujenzi wa Soko la ghorofa Kata ya Mbagala Kuu**
- **Ujenzi wa Soko Kata ya Mtoni**
- **Ujenzi wa Soko la ghorofa Kata ya Kilakala**
- **Ujenzi wa Soko la ghorofa Kata ya Makangarawe**
- **Ujenzi wa Soko la ghorofa Kata ya Mbagala**

**VI. Ujenzi wa Vituo vya Daladala**

- **Ujenzi wa kituo cha daladala Kata ya Kijichi**
- **Ujenzi wa kituo cha daladala Kata ya Mbagala Kuu**
- **Ujenzi wa kituo cha daladala Kata ya Mtoni**
- **Ujenzi wa kituo cha daladala Kata ya Kilakala**
- **Ujenzi wa kituo cha daladala Kata ya Makangarawe**
- **Ujenzi wa kituo cha daladala Kata ya Mbagala**

**VII. Ununuzi wa magari 10 ya kuzolea & kusafirishia takataka**

**VIII. Maandalizi ya Mji wa Kisasa**

- **Halmashauri inatarajia kupima viwanja 1000 na kuviwekea miundombinu msingi.**

**IX. Ujenzi wa uwanja wa michezo eneo la Makangarawe**

- **Halmashauri inatarajia kujenga uwanja wa michezo wenye hadhi ya kimataifa**

Kutoka Uk. 12

- **UTEKELEZAJI WA MRADI**

**MRATIBU** wa mradi huo katika Manispaa hiyo, Mkerewe Tungaraza, anasema mradi huo ulianza kutekelezwa rasmi mwaka 2016.

Anasema mradi huo umelenga maeneo manne ambayo ni uboreshaji wa maeneo ya manispaa hiyo na ujenzi wa miundombinu.

Anasema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 73.2 na kwamba watajenga kilometa 27 za barabara za mitaa mbalimbali zinazounganisha barabara kuu.

Tungaraza anasema moja ya kazi kubwa ambayo itafanywa ni kuboresha mto ng'ombe ili maji yasituame hovyo na kuleta madhara kwa wananchi wanaoishi kando kando.

Anasema pia wataboresha makazi ya watu, kukarabati mifereji na kuwa katika kiwango cha kimataifa.

"Awamu ya kwanza imeanza kwa kufanya kazi kwenye mto ng'ombe ambao utagharimu Sh. bilioni 40 na halmashauri imeshatenga Sh. bilioni 1.7 kwa ajili ya fidia kwa wakazi wa maeneo yanayopitiwa na mradi," anasema.

Anasema awamu ya kwanza ni kufunga taa za barabarani kwenye ujenzi wa barabara zenye urefu wa kilometa 7.5 unaendelea.

Ujenzi wa ofisi ya kudumu na kuweka samani na ujenzi wa maabara ya kisasa yenye vifaa vya kupima ubora wa kazi nayo inaendelea.

Anasema miradi ya awamu ya kwanza inatarajiwa kukamilika Januari 13, mwaka 2018 na kwamba awamu nyingine zitaendelea.

Anasema pia watajenga vioski kwa ajili ya maji na vyoo vya kulipia maeneo yenye msongamano mkubwa wa watu.

Kuhusu barabara ya makumbusho anasema itagharimu Sh. bilioni 1.45 na barabara ya kuelekea viwandani Sh. bilioni 2.1.

Tungaraza anasema, barabara ya makumbusho ipo katika hatua za mwisho za kukamilika na kwamba kazi iliyobaki ni kufunga taa na kuweka matuta.

Pia anasema kuna ujenzi wa barabara ya Mabibo Jeshini ambayo Mkandarasi ameshaanza kazi ambayo itajengwa kwa kilometa 2.8 na barabara ya Kisukuru kuelekea Kilungule itakayojengwa kwa urefu wa Kilometa 1.9.

Kuhusu barabara ya Mwanayamala, Mburahati na Tandale watafanya uboreshaji wa miundombinu.

Kuhusu barabara ya makumbusho anasema itagharimu Sh. bilioni 1.45 na barabara ya kuelekea viwandani Sh. bilioni 2.1.

Tungaraza anasema, barabara ya makumbusho ipo katika hatua za mwisho za kukamilika na kwamba kazi iliyobaki ni kufunga taa na kuweka matuta.

Pia anasema kuna ujenzi wa barabara ya Mabibo Jeshini ambayo Mkandarasi ameshaanza kazi ambayo itajengwa kwa kilometa 2.8 na barabara ya Kisukuru kuelekea Kilungule itakayojengwa kwa urefu wa Kilometa 1.9.

Kuhusu barabara ya Mwanayamala, Mburahati na Tandale watafanya uboreshaji wa miundombinu.

- **WANANCHI WANUFAIKA**

Naye Ofisa Ustawi wa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, Pendo Mwaisaka, alisema kazi wanayofanya katika mradi huo ni kuhakikisha shughuli zinazofanyika hazina madhara kwa wananchi.

Anasema jamii inatakiwa kuufahamu mradi huo, kuhoji kuhusu shughuli zinazofanyika na kutoa malalamiko yao pindi mradi huo unafanyika.

Mwaisaka anasema, walifanya vikao na wananchi kabla ya kuanza mradi huo na kwamba wanaendelea kushirikiana na jamii hadi utakapokamilika.

"Licha ya kuwa mradi huu unatelekezwa na serikali, sisi kama maofisa ustawi wa jamii tunahakikisha jamii inahusishwa moja kwa moja lakini pia inashughulikia changamoto zao," anasema.

Mwaisaka anasema wakati wa ujenzi wa barabara wanahakikisha wananchi hawapatwi na madhara ya aina yoyote.

Anasema jumla ya wananchi 99 waliokuwa wakiishi kando ya barabara waliondolewa na walisimamia kuhakikisha wanalipwa stahiki zao.

Anasema baada ya kulipwa fidia pia waliwashauri wananchi wazitumie kwa ajili ya manufaa yao na kuboresha makazi yao na si vinginevyo.

# Mradi wa DMDP Kuwaondolea Kero ya Maeneo Wamachinga

***Na Mwandishi wetu***

**UFANYAJI** biashara ndogondogo(umachinga) ni fursa mbayo ikitumika vyema,itatengeneza ajira kwa vijana wengi wanaokabiliwa na changamoto ya ukosefu wa kazi.

Hata hivyo yapo mambo yanayowezesha kugeuza umachinga kuwa fursa ikiwa ni pamoja na kuanzisha madirisha maalum kwa mikopo nafuu ya kuimarisha mitaji ya wafanyabiashara hao.

Lingine na kubwa zaidi ni upatikanaji wa uhakika wa masoko au sehemu za kufanyia shughuli zao.

Kwa kutambua umuhimu wa kundi hili, Serikali ilibuni mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es salaam(DMDP) kwa dhamiri ya kupambana na changamoto zikiwemo za kuondoa umasikini na kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira hasa kwa vijana ambao ni kundi muhimu katika Taifa hili.

Kadhalika , kundi hili la jamii linahitaji kujengewa uwezo ili lichangie katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii ipasavyo.

Mradi huu unaotekelezwa katika Manispaa tatu za Jiji la Dar es Salaam ambazo ni Temeke, Ilala na Kindondoni utaboresha miundombinu ya barabara , kupandisha hadhi ya maeneo yaliyojengwa kiholela kwa kupeleka huduma za ukusanyaji wa taka ngumu, kujenga maeneo ya kupumzikia, ujenzi wa masoko, huduma za vyoo vya Umma pamoja huduma ya maji safi.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI Mhe.Selemani Jafo amesema moja ya miradi unaotekelezwa kupitia DMDP ni ujenzi wa masoko tisa ya kisasa katika Manispaa zote tatu ambayo yatakayotatua changamoto za wafanyabiashara ndogondogo

“Tunakwenda kujenga masoko, mfahamu katika Jiji hili wamachinga wamesambaa, na tatizo kubwa ni maeneo ya kufanyia biashara. Nimebahatika kutembelea soko la Ilala, Temeke, Buguruni, Temeke Sterio, Pugu Kajiungeni, tatizo la ukosefu wa maeneo kwa wamachinga kufanya shughuli zao ni kubwa na hali ni mbaya.

“Leo hii nimetembelea Mbagala pamoja na kuwa tulijenga miundombinu ya barabara, nyakati za jioni utakuta wamewek vifurushi pale, nguo, viatu, nyanya na vitu mbalimbali ambavyo vinachangia katika uharibifu wa barabara, sasa kupitia Mradi huu tunakwenda kuboresja Jiji la Dar es salaam katika maeneo ya kiuchumi ambayo yatalenga wafanyabisahara ndogondogo” anasema Jafo.

Jafo anaongeza, “uchumi tunaoulenga ni ule wa chini, na wa kati na katika hilo masoko yatakayojengwa yatakuwa ya kisasa ili kuwezesha shughuli za wamachinga na kuwafanya wapate fursa ya kuuza bidhaa zao bila bughudha na waweze kuchagua wapi wanaweza kwenda kufanya biashara zao.

Pia tutapunguza hata ajali zinazotokana na wamachinga kufanya biashara barabarani na kandokando ya barabara”.

Jafo anatumia fursa hii kuwahimiza wakurugenzi na wasimamizi wa miradi hiyo. “Katika miradi hii sitotaka masihara, nataka nione thamani ya Fedha”.

**MANISPAA YA ILALA**

Mkurugenzi wa Manispaa ya Ilala, Msongela Palela anasema kwa kushirikiana na wadau wengine

**Inaendelea Uk……… 19**



*Wafanyabiashara ndogondogo wakifanya biashara zao katika eneo la barabara kinyume na taratibu*

# DONDOO MUHIMU ZA MRADI ZA DMDP

## MANISPAA YA KINONDONI

i. Ujenzi wa barabara

A. Sokoni Makumbusho Km 1.45, Nzasa Km 1.25,, Viwandani Km 2.10, Tanesco-Soko la Samaki Km 1.6

B. Makanya Km 5.1, Tandale –Kisiwani Km 0.4, Kilimani Km 1.3, Simu 2000 Km 1.3, Kilongawima Km 1.8 na CBD Makumbusho Km 2.85

C. External Km 2.65, Kisukuru Km 1.9, Korogwe-Kilungule Km 2.88 na Maji ya Chumvi-Kilungule Km 2.85.

D. Shekilango Km 3.8

E. Magomeni Mapipa Km 6.58

F. Makumbusho-Mwanamboka Km 4.08 na Muhimbili Km 1.34

G. Morroco –Kawe Km 7.74

Ii. Ujenzi wa Ofisi ya Mradi pamoja na Maabara

Iii. Ujenzi na uboreshaji wa Mto Sinza Km 7.5

Iv. Uboreshaji wa Makazi yasiyopangwa katika Kata Nne

## MANISPAA YA ILALA

I. Ujenzi wa barabara sita za Ndanda, Olimpio,Kiungani, Omari Londo, Mbaruku na Kongo Km 2.9

II. Ujenzi wa Miundombinu ya mafuriko na mifereji ya maji ya mvua katika maeneo ya Buguruni Kisiwani,Tenge,Luwiti,Bondela Sungura na Tembo Mgwaza Km 6.14

III. Ujenzi wa miundombinu ya mafuriko na mifereji ya maji ya mvua katika maeneo ya Temeke,Mto Mpogo, Minazi mirefu, Kigilagila na Kiwalani Urefu wa Km 9.8

IV. Ujenzi wa barabara Tano katika Kata ya Gongolamboto ambazo ni Chunge,Kampala,Limbanga,Mlima mrefu na Bagdad Km 7.8 pamoja na ujenzi wa mifereji ya maji ya mvua Km 1.8 pamoja na ununuzi wa vifaa vya kukusanyia na kubebea Taka

V. Ujenzi wa barabara Tano katika Kata ya Kiwalani ambazo ni bush,Gude,Jongo,Mbilinyi,Pepsi,Jamaka,Zahanati,Kamungu,Mkwajuni,Binti Musa na Betherl Km 10.3

VI. Ujenzi wa barabara Tano za Mrisho katika kata ya Ukonga ambazo ni Markaz,Zimbili,Zahanati,Shule na Chacha Km 11.2

Kutoka Uk.17

**WANATAKA** kuboresha mapato kwa kuwa na miradi shirikishi hasa kwenye kata za Manispaa ya Kinondoni.

"Masoko haya yatajengwa sehemu ambazo kuna uhitaji na msongamano mkubwa wa wafanyabishara hivyo kutakua na fursa za biashara katika maeneo ya jirani na wananchi hivyo itakua sio lazima tena wananchi kuja katikatika ya Mji kufuata mahitaji muhimu na hii iitapunguzia wananchi adha ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma.

Pia itachangamsha maeneo tutakayoweka hivyo vyanzo vya mapato na pia itasaidia kupunguza msongamano katikati ya mji,

**MANISPAA YA KINONDONI**

Meya wa Manispaa ya Kinondoni Benjamini Sitta anasema watajenga barabara kuzunguka masoko jambo litakaloongeza thamani ya biashara ambayo moja kwa moja italeta afya kwa wafanyabiashara katika maeneo hayo.

"Mradi huu ni neema kubwa hususan kwa wafanyabiashara ndogondogo, ninaishukuru Serikali kwa kuja na kipengele cha kujenga masoko ya kisasa".

"Vijana wetu sasa watakua na ameneo ya uhakika ya kufanyia shughuli zao za kujiingizia kipato" anasema.

Hussein Juma ni dereva wa dalaldaa inayofanya safari zake kati ya Makumbusho na Bunju anasema maboresho yaliyofanywa yamewapunguzia gharama za uendeshaji wa daladala hizo.

"Kwa kweli ilikua shida kuingia katika kituo hiki. Tulikua tunatumia fedha nyingi kubadilisha vifaa vilivyokuwa vikiharibika kutokana na ubovu wa barabara" anasema.

Julieth Hamprey, mfanyabiashara katika eneo la Makumbusho anasema maboresho yaliyofanywa na Serikali yamewaongezea uhakika wa kufanya biashara kwa kuwepo wateja wengi.

"Tunashukuru kwa maendeleo haya tuliyoletewa, ingawa kila maendeleo yanaambatana na machungu kiasi, kwani wenye maduka wametupandishia kodi. Kupanda kwa kodi hakututii shaka sana kwa sababu sasa nina uhakika wa kufanya biashara vizuri" anasema.

**MANISPAA YA TEMEKE**


Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke, Nasib Mbaga anasema kwa upande wa Manispaa yake mradi huu unalenga kuboresha masoko manne yatakayotumiwa na wananchi wa maeneo imara ya kukusanya mapato.

Naye Meya wa Temeke, Abdalah Chaurembo anasema kukamilika kwa mradi huu kutapunguza kero na adha kubwa ambazo wananchi walikuwa wakizipata.

"Mradi huu utapunguza msongamano wa watu katikati ya Jiji kwa sababu utawezesha huduma kuwafuata walipo na kwamba uhalifu pia utapungua katika ameneo hayo.

Watu walikuwa wanaenda mjini kwa shughuli ndogondogo kwa sasa lengo la mradi huu unawasogezea wananchi huduma.

Hivyo ukikamilika wananchi watapata mahitaji walipo na mlolongo wa watu kwenda mjini bila sababu utapungua" anasema Chaurembo.




**Ujenzi wa barabara ya Makumbusho uko katika hatua ya ukamilishaji na wananchi wamekwishaanza kufurahia faida za mradi wa *DMDM***

# Picha mbalimbali zikionyesha hali ya miundombinu katika Manispaa ya Temeke kabla na baada ya Ujenzi

*Picha na Rafael Kilapilo, OR-TAMISEMI*

OR-TAMISEMI

DMDP
Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam







**Ujenzi wa Darala la Kijichi-Twangoma kupitia mradi wa DMDP**

www.tamisemi.go.tz

OR-TAMISEMI

DMDP
Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam







**Ujenzi wa Kalavati kwenye barabara Kijichi-Twangoma kupitia mradi wa DMDP**

www.tamisemi.go.tz

# Picha mbalimbali zikionyesha hali ya miundombinu katika Manispaa ya Temeke kabla na baada ya Ujenzi

*Picha na Rafael Kilapilo, OR-TAMISEMI*

OR-TAMISEMI

DMDP

Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam



KABLA



BAADA

**Ujenzi wa barabara ya Kijichi-Twangoma iliyojengwa kupitia mradi wa Uboresaji wa Jiji la Dar es Salaam "DMDP".**

www.tamisemi.go.tz

OR-TAMISEMI

DMDP

Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam



KABLA



BAADA

**Ujenzi wa barabara ya Mwanamtoti-Temeke maarufu kama barabara ya Ng'ombe iliyojengwa kupitia mradi wa DMDP**

www.tamisemi.go.tz



JENGO LA MRADI WA DMDP MANISPAA YA ILALA




JENGO LA MRADI WA DMDP MANISPAA YA KINONDONI